

Jinsi ya Kushiriki?

Wasiliana na Kundi Andalizi la Kitaifa katika nchi yako ili uweze kushiriki katika maandalizi ya Harakati ya 2010 ya Wanawake. Maelezo zaidi yaweza kupataikana kupitia mtandao:

<http://www.marchemondiale.org/structure/cn-groupes/en/>

Tayari kuna harakati zimeandaliwa katika mwaka wa 2009 kama matayarisho ya Harakati ya mwaka wa 2010 za ulimwengu:

- Mikutano ya kimajimbo na kikanda kwa madhumuni ya kuandaa kwa undani zaidi mipango katika nchi zinazopatikana katika maeneo husika.
- Maandalizi kuwahusisha makundi na washirika mbalimbali juu ya harakati zitakazofanywa sambamba katika sehemu tafautitfauti duniani.
- Kufafanua hatuwa muhimu za kipaumbele kuchukuliwa kitaifa na zile za ki-kanda ili kupata mafanikio madhubuti.

Ikiwa hakuna Kundi la Kitaifa pale ulipo, wasiliana na Ofisi Kuu Andalizi ya Harakati za Wanawake movilizacion@marchemondiale.org au Wanachama wa Kimataifa wanaopatikana katika eneo ulipo.

Badilisha maisha ya wanawake
ubadilishe ulimwengu!
Badilisha ulimwengu ubadilishe
maisha ya Wanawake!



Kwa Maelezo zaidi?

Afisi Kuu Ya Kimataifa ya Harakati za Wanawake Duniani

Rua Ministro Costa e Silva, 36
Pinheiros • CEP 05417-080
São Paulo • SP
Brasil

Simu +55 11 3032-3243

Fax +55 11 3032-3239

Barua Pepe: info@marchemondiale.org

Site: www.marchemondiale.org



Awamu ya Tatu ya Harakati za Wanawake

Kimataifa

Machi 8 hadi

Oktoba 17



Wanawake tu kwenye Harakati hadi tuwe huru!

"Harakati za Wanawake Duniani" ni kikundi cha kimataifa kinachounganisha makundi yaliyoko mashinani pamoja na mashirika mbalimbali kwa madhumuni ya kuangamiza umasikini na dhulma dhidi ya wanawake.



Wakati wa shughuli za Harakati za Wanawake Duniani...

...Ni wakati wa kuzidisha nguvu harakati zetu. Kuwa "katika harakati" ni dhahirisho kuwa tunasonga mbele tukiungana pamoja kama mashirika na makundi mbalimbali za wanawake kwa na niya ya kuwa huru hatimae. Zaidi ya hayo, ni dhahirisho la nguvu zetu kama wanawake, japo tuna ujuzi mbalimbali kiasiasa, kitamaduni na kadhalika, lengo ni moja – ile ya kuangamiza mfumo wa dhulma unaohimiza na kuelekeza tu kwenye ukandamizaji na umasikini. Katika malengo yetu pia, ni umoja wetu kwa madhumuni ya kuonyesha umoja katika yanayowakabili madada wenzetu walioko katika sehemu nyengine za dunia.

Katika mwaka wa 2010, tutazidi kupaaza sauti zetu kwa mshindo mkuu ulimwengu mzima kuanzia Machi 8 hadi Octoba 17. Harakati zetu zitatekelezwa katika vipindi viwili kama ifuatavyo:

- Kuanzia **Machi 8 hadi 18** kutakuwa na maandamano aina kwa aina, rangi na nyimbo, ambay pia yataadhimisha miaka mia tangu kutangazwa Siku ya Wanawake Duniani;
- **Octoba 17** kutakuwa na maandamano sambamba katika sehemu tafauti tafauti. Mkutano rasmi utafanyika katika mji wa Bukavu, mkoa wa Kivu Kusini, Jamhuri ya Democrasia ya Congo, ili kudhirisha umuhimu na mchango wa wanawake kama kiungo muhimu katika kutatua matatizo yanayokumba maeneo ya vita.

Maudhui ya shughuli za 2010 itaongozwa na misingi minne ya Harakati za Wanawake Duniani:

Haki za Kimsingi. Kupinga ubinafsishaji wa huduma za umma. Tunasisitiza kuwa na haki za kupata chakula, afya, elimu, maji na usafi ni lazima maishani.

Amani na kuangamizwa kwa silaha. Tunafanya juhudi za kudhirisha undani na sababu za vita miongoni mwazo ni vipi kuathiriwa kwa maisha ya wanawake. Katika mazingira haya pia, kuonyesha ni vipi ukabila, dini pamoja rasimili na maslahi ya wafanyabiashara wa silaha kunatumia kuchochea vita.

Ni yapi maudhui ya kushughulikiwa?

Wakiwa mikononi mwa wanajeshi au makundi yenye silaha, wanawake wengi hupata shida nyakati za kubakwa na hasa baada ya visa hivyo kutendeka, wengi wao hakataliwa na jamii huku wakilaumiwa kwa shida zilizowapata.

Kazi za wanawake. Tunawatetea wake kwa waume ili waweze kupata huduma sawa za kisheria, haki za jamii na ajira sawa kote ulimwenguni bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Dhulma dhidi ya wanawake. Tunapinga dhulma dhidi ya wanawake kupitia juhudi za kuelimisha jamii, makundi ya harakati na kuwasilisha madai kwa mataifa. Ni lengo letu kufafanua ni vipi dhulma hizo hutoka na sababu zake ni zipi na kusimama imara kuonyesha kupinga kudhulumiwa kwa wanawake kijinsia.

Tutatumia Mifumo ipi ya Harakati?

Kila kikundi cha kitaifa kina uhuru wa kufafanua mfumo ufaao katika Harakati ya 2010. Miongoni mwa mifumo iliyopendekezwa ni:



- Maandamano ya siku kumi kupitia barabara maalum.
- Misafara ya bas na treni huku kukiwa kumepangwa vipindi vya mihadhara njiani.
- Maonyesho ya sanaa na ya kitamaduni kama vile michezo ya kuigiza, filamu na vikao vya kuandaa mijadala kuhamasisha kampeni ya Harakati.
- Maandilizi ya maandamano zitakazofanywa kimitaa kwa madhumuni ya kuunga mkono juhudi za Harakati za Wanawake katika maeneo na nchi mbalimbali.
- Maandamano katika maeneo kunakotengezwa silaha au nje ya afisi za waakilishi wao. Kwengine ni mbele ya afisi za Umoja wa Mataifa.
- Kampeni kususia bidhaa kutoka kwa makampuni yanazohusika na uporaji na kufaidika kutokana na manufaa ya vita.

